# BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

Simu Nam. + 255 24 2230602/1
Fax Nam. + 255 24 2230215
Tovuti: www.zanzibarassembly.go.tz

SANDUKU LA BARUA 902,
ZANZIBAR
Barua Pepe: zahore@zanlink.com

## HOTUBA YA MAONI YA KAMATI YA KUCHUNGUZA NA KUDHIBITI HESABU ZA SERIKALI ZA MITAA NA MASHIRIKA (LAAC) KUHUSIANA NA UWASILISHAJI WA RIPOTI YA OFISI YA RAIS, FEDHA NA MIPANGO KUHUSU RIPOTI YA UTEKELEZAJI WA MAONI, USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI YA LAAC KWA MWAKA 2018/2019 NA 2019/2020

**Mheshimiwa Spika,** naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu Muumba Mbingu na Ardhi kwa kutujaalia uzima na afya njema na kutuwezesha kukutana hapa leo kwa ajili ya kutekeleza majukumu yetu muhimu ya kikatiba ya kuisimamia Serikali na kuwawakilisha wananchi wa Zanzibar ndani ya Muhimili huu muhimu wa nchi yetu.

Aidha, nikushukuru wewe Mheshimiwa Spika kwa kuniruhusu kusimama mbele ya Baraza lako Tukufu kwa niaba ya Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali za Mitaa na Mashirika kuwasilisha machache kuhusiana na Uwasilishaji wa Ripoti ya Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango kuhusu Ripoti ya Utekelezaji wa Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya LAAC kwa mwaka 2018/2019 na 2019/2020.

**Mheshimiwa Spika,** sina budi kumpongeza Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango - Mheshimiwa Dkt. Saada Mkuya Salum, watendaji wa Wizara hii pamoja na watendaji wote wa Taasisi zilizotajwa kwenye Ripoti ya Utekelezaji wa Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati hii iliyowasilishwa hivi punde na Mheshimiwa Waziri kwa mashirikiano yao waliyotupatia wakati wote wa kuipitia na kuijadili Ripoti hiyo.

**Mheshimiwa Spika,** kwa namna ya pekee, nawapongeza na kuwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali za Mitaa na Mashirika, kwa umahiri na umakini wao mkubwa waliouonesha wakati wa kuipitia na kuijadili Ripoti ya Utekelezaji wa Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati na hatimae kuandaa Hotuba ya Kamati kuhusiana na Ripoti hiyo.

**Mheshimiwa Spika,** Pongezi na shukrani hizi pia ziende kwa Makatibu wa Kamati hii kwa ushauri na maelekezo yao ya kitaalamu yaliyowawezesha Wajumbe wa Kamati kutekeleza jukumu lao hili kwa wepesi na kwa ufanisi mkubwa.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa umuhimu wao huo, na kwa ruhusa yako naomba niwatambue Wajumbe na Makatibu wa Kamati yetu kama ifuatavyo:

1. Mhe. Habib Ali Muhamed - Mwenyekiti;
2. Mhe. Mwanaasha Khamis Juma - Makamo Mwenyekiti;
3. Mhe. Bakar Hamad Bakar - Mjumbe;
4. Mhe. Haji Shaaban Wazir - Mjumbe;
5. Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa - Mjumbe;
6. Mhe. Shadya Mohamed Suleiman - Mjumbe;
7. Ndg. Nasra Awadh Salmin - Katibu; na
8. Ndg. Yussuf Mkamba Mwinyi - Katibu.

**Mheshimiwa Spika,** hatuna budi pia, kuwashukuru na kuwapongeza kwa dhati waliokuwa Wajumbe wa Kamati ya LAAC Mheshimiwa Shaibu Hassan Kaduara na Mheshimiwa Shamata Shaame Khamis kwa mashirikiano yao makubwa waliyoipatia Kamati hii.

**Mheshimiwa Spika,** Wajumbe wako hawa kwa kiasi kikubwa walichangia kutoa Maoni, Ushauri na Mapendekezo ambayo leo hii yanawasilishwa utekelezaji wake na Serikali.

**Mheshimiwa Spika,** tunawaombea dua kwa Mwenyezi Mungu azidi kuwaongoza katika kutekeleza majukumu yao ya Kitaifa, Aamiin.

**Mheshimiwa Spika,** kiujumla Kamati ya LAAC inaipongeza Serikali kwa kuyakubali na kuyatekeleza kwa asilimia kubwa Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati hii waliyoyatoa kwa dhamira ya kujenga nchi yetu.

**Mheshimiwa Spika,** kitendo hiki kimekipa sana faraja Kamati na kimeonesha umahiri na weledi mkubwa waliokuwa nao Wajumbe wa Kamati ya LAAC.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ya LAAC inalipongeza Shirika la Bandari kwa kuanza kutekeleza kwa vitendo na kuona tija yake pendekezo la Kamati la kufunga hesabu za mwisho wa mwaka na kwa upande wa Pemba pekee (Segment Report) ili Shirika kuweza kupima utendaji wa bandari kwa Pemba.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ya LAAC ilitoa pendekezo hilo kwa kuwa asilimia kubwa ya Taasisi za Pemba hesabu zake huwa hazijulikani kwa kuwa zinajumuishwa moja kwa moja kwenye hesabu kuu ya Taasisi jambo linalokwaza kuweza kupima utendaji wa Taasisi hizo kwa upande wa Pemba.

**Mheshimiwa Spika,** kwa mnasaba huo, Kamati ya LAAC inazidi kuzishauri na Taasisi nyengine kuweza kutekeleza jambo hilo muhimu kwa maendeleo ya Taasisi zao kutokana na sababu ilizozieleza.

**Mheshimiwa Spika,** hivyo, katika mwaka wa fedha kutakuwa na hesabu tatu kama ifuatavyo:

1. Hesabu kwa ajili ya Unguja pekee;
2. Hesabu kwa ajili ya Pemba pekee;
3. Hesabu itakayojumuisha taarifa za Unguja na Pemba kwa ujumla.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ya LAAC inalipongeza Shirika la Bandari kwa kuweza kununua mizani nne katika mwaka wa fedha 2021/2022 kama lilivyoahidi mbele ya Kamati baada ya Kamati kupendekeza kununuliwa mizani hizo kwa kuwa mizani iliyokuwepo wakati Kamati inafanya ziara Bandarini hapo tarehe 18 Agosti, 2021 haikuwa rafiki kwa kuweza kupima kila aina ya gari inayobeba mizigo.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na pongezi hizo, Kamati ya LAAC inalishauri Shirika la Bandari kuzisimamia vyema mizani hizo ili ipatikane tija ya kununuliwa kwake huko pamoja na kuzitunza ili ziweze kutumika kwa muda mrefu na kuepuka kuitia hasara Serikali.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ya LAAC, inaipongeza Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango kwa kuanza kulipa deni la mkopo la fedha za Kitanzania Bilioni Moja nukta Tano (Tsh. 1.5 Bilioni) ikiwa ni malipo ya mkopo wa fedha za Kitanzania Bilioni Ishirini na Saba, Milioni Nane na Sitini na Mbili na Laki Tano (Tsh. 27, 862,500,000) zilizotolewa kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za Kwahani na Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (ZSSF).

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ya LAAC inazidi kuisisitiza Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango kulipa mkopo wa fedha hizo kwa mujibu wa mkataba hasa ikizingatiwa kuwa fedha hizo ni haki ya wanachama wa Mfuko huo fedha ambazo kwa sababu yoyote ile ya kisheria mwanachama husika hupaswa kulipwa endapo itatokea haja hiyo, hivyo, ni busara fedha za Mfuko zikawepo muda wote.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ya LAAC imefarijika baada ya kutaarifiwa na Shirika la Meli na Uwakala kuwa pendekezo la Kamati la kuuzwa kwa Meli ya MV. Maendeleo na MT. Ukombozi tayari limefanyiwa kazi kwa meli hizo kupata wanunuzi.

**Mheshimiwa Spika,** kwa msingi huo, napenda kuliarifu Baraza lako Tukufu kuwa Meli MV. Maendeleo itauzwa kwa fedha za Kimarekeni Laki Mbili na Thalathini Elfu (230,000) na Meli ya MT. Ukombozi itauzwa kwa fedha za Kimarekani Laki Mbili na Hamsini na Moja Elfu (251,000).

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ya LAAC inaunga mkono suala hilo kwani ilikuwa ikisikitishwa sana na taarifa zinazotolewa na Shirika hili na Kamati yako ikajiridhisha kuwa meli hizo hazina tija na zinaitia zaidi hasara Serikali.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ya LAAC inalishauri Shirika la Meli na Uwakala kuendelea na jitihada za kutafuta Kampuni za Tanzania Bara ili kuzishawishi kuingia nazo ubia na kujenga jengo la ghorofa badala ya kuendelea kumiliki nyumba ambazo hazina tija kwa kuwa Taasisi za SMZ ambazo zinafanya kazi Tanzania Bara, hazipo tayari kutekeleza suala hilo kwa sasa.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ya LAAC haipingani na majibu ya Serikali kuhusiana na utekelezaji wa pendekezo lake ililolitowa kwa Mamlaka ya Mafunzo ya Amali juu ya kuachiwa Mamlaka hiyo kutekeleza na kusimamia miradi yake badala ya jambo hilo kutekelezwa na Wizara inayosiamamia Mamlaka hiyo kwa kuwa ndio Sera ya Serikali. Hata hivyo, Kamati ya LAAC inaiomba Serikali endapo itatekeleza suala kama hilo kuzidi kuwa karibu na Taasisi husika ili kuepuka kuingia hasara.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ya LAAC inasisitiza hilo kwa kuwa Mamlaka ya Mafunzo ya Amali mradi wake ulisimamiwa na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali na kununuliwa vifaa vyenye thamani ya fedha za Kitanzania Milioni Mia Moja na Kumi na Nane, Laki Tisa, Elfu Moja na Sabini na Tisa (Tsh. 118,901,079) vifaa ambavyo vilihifadhiwa muda mrefu bila matumizi na hatimae kuripotiwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuwa ni hoja, kitu ambacho hakileti taswira nzuri kiutendaji.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ya LAAC haipingani na njia iliyotumiwa na Serikali ya kulipa deni la fedha za Kitanzania Bilioni Tatu, Milioni Mia Mbili na Sabini na Mbili, Laki Sita na Elfu Tatu (Tsh. 3,272,603,000) la Mfuko wa Barabara wanaloidai Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango. Hata hivyo, Kamati ya LAAC inaishauri Serikali kulifuta deni hilo ili lisisomeke tena kwenye hesabu za Mfuko wa Baraza kwa lengo la kupatikana usahihi wa taarifa za hesabu za fedha na kuiepushia Taasisi hii kupata hoja isiyo na msingi.

**Mheshimiwa Spika,** kabla ya kumaliza hotuba hii naomba kuzitahadharisha Taasisi zilizopo chini ya Kamati hii kuwa Kamati ya LAAC kwa mujibu wa Jadweli la Pili la Kanuni za Baraza la Wawakilishi, Toleo la 2020 ina wajibu wa kufuatilia majibu ya utekelezaji wa maagizo yake. Hivyo, Kamati hii inaliahidi Baraza hili kuwa itafuatilia kwa karibu majibu hayo na kuthibitisha juu ya kile kilichoelezwa kama ni sahihi.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ya LAAC inalisema hili kwa kuwa miongoni mwa Kamati yako iliwahi kufuatilia majibu ya utekelezaji wa maagizo yake na kubaini kuwa hakuna chochote kilichofanywa na Taasisi hiyo na hatimae kubakia kuomba radhi tu.

**Mheshimiwa Spika,** kwa mnasaba huo, Kamati ya LAAC inawaasa Watendaji Wakuu wa Taasisi zilizopo chini yake kupitia Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango lisitokee jambo kama hilo kwa maslahi ya wananchi na taifa kwa ujumla.

**Mheshimiwa Spika,** naomba nimalizie kwa kuwashukuru Wajumbe wote wa Baraza hili, kwa utulivu wao na kwa kunisikiliza kwa makini wakati wote nilipokuwa nawasilisha maoni ya Kamati ya LAAC kuhusiana na Uwasilishaji wa Ripoti ya Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango kuhusu Ripoti ya Utekelezaji wa Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya LAAC kwa mwaka 2018/2019 na 2019/2020.

**Mheshimiwa Spika,** naomba kuwasilisha.

……………………

Habib Ali Mohamed,
Mwenyekiti,
Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali za Mitaa na Mashirika (LAAC),
Baraza la Wawakilishi,
**Zanzibar.**